SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI (AFISI YA RAIS) KATIBA NA UTAWALA BORA, MHESHIMIWA BRIG. GEN. (Mst.) ADAM C. MWAKANJUKI KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NCHI (AR) KATIBA NA UTAWALA BORA KWA MWAKA WA FEDHA 2004/2005

June 2004

HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI (AFISI YA RAIS) KATIBA NA UTAWALA BORA, MHESHIMIWA BRIG. GEN. (Mst.) ADAM C. MWAKANJUKI KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NCHI (AR) KATIBA NA UTAWALA BORA KWA MWAKA WA FEDHA 2004/2005

YALIYOMO

		Ukurasa
1.	Utangulizi	1 – 2
2.	Utekelezaji wa Kazi kwa Mwaka wa Fedha 2003/2004	
3.	Muundo wa Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora	
4.	Idara ya Utawala na Uendeshaji	
5.	Kamisheni ya Wakf na Mali ya Amana	
6.	Idara ya Mahkama	
7.	Idara ya Mrajis Mkuu wa Serikali	
8.	Idara ya Mufti wa Zanzibar	
9.	Idara ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali	
10.	Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Kusimamia Maadili ya Viongozi	
11.	Idara ya Kuratibu Shughuli za Utawala Bora	
12.	Idara ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP)	
13.	Idara ya Mwanasheria Mkuu	
14.	Afisi Kuu Pemba	
15.	Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka 2004/2005	
16.	Mwisho	
17.	Viambatisho	

HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI (AFISI YA RAIS) KATIBA NA UTAWALA BORA, MHESHIMIWA BRIG. GEN. (Mst.) ADAM C. MWAKANJUKI KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NCHI (AR) KATIBA NA UTAWALA BORA KWA MWAKA WA FEDHA 2004/2005

UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu sasa liingie katika Kamati ya Matumizi ili liweze kujadili na hatimae kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nchi (Afisi ya Rais) Katiba na Utawala Bora ya Mwaka wa Fedha 2004/2005.

2. Mheshimiwa Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uzima, kuweza kufika tena hapa leo hii kuendelea na shughuli yetu muhimu kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. Tunaomba Mwenyezi Mungu atuzidishie hikma, busara na atupe muelekeo mwema na mashirikiano mazuri zaidi ili tuweze kufanikisha jukumu letu vizuri.

3. Mheshimiwa Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea na usimamizi wa ujenzi wa umoja na uchumi wa Zanzibar kama ambavyo Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2000 ilivyoelekeza.

4. Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii pia kumpongeza Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha katika kazi zake za usimamizi wa siku hadi siku wa shughuli za Serikali. Ni dhahir kwamba juhudi zake na ukweli wake umelenga kuugomboa umma wa Zanzibar kuondokana na umasikini hasa katika dunia hii inayobadilika kila kukicha.

5. Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa ufanisi wako na uwajibikaji wako katika kazi yako na katika shughuli mbalimbali za kijamii. Uwezo wako ndani na nje ya nchi umeonesha kuwa majukumu uliyopewa kweli unaweza kuyatimiza. Sambamba na hilo nawapongeza wajumbe wako wote wa Baraza lako hili kwa kuendelea kusimamia juhudi za kuleta maendeleo kwa wananchi na nchi yao, aidha kwa kuimarisha ujenzi wa Misingi ya Utawala Bora. Pia nawapongeza na kuwashukuru wajumbe wako wote waliochangia hotuba ya Wizara yangu

katika mwaka wa fedha 2003/2004. Hakika michango yao imewezesha Wizara yangu kutekeleza vyema majukumu yake.

6. Mheshimiwa Spika, pongezi na shukrani maalum nazitoa kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza lako tukufu chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Ali Juma Shamhuna kwa ushauri wao, maelekezo yao na busara zao kwa wakati wote. Michango na maelekezo yao yametusaidia mimi na watendaji wa Wizara yangu kuwa makini katika utendaji na utekelezaji wa majukumu na malengo tuliyojiwekea.

7. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatoa pongezi kwa umma wote wa Zanzibar kutokana na kuendelea kulinda hali ya amani na utulivu nchini mwetu, vitu ambavyo vinadumisha udugu wetu. Hata hivyo tunalaani kwa nguvu zote vitendo vya wachache wenye lengo la kuvuruga amani waliojihusisha na uripuaji wa mabomu. Tunaamini kuwa sisi ni wamoja na hakukuwa na haja ya kufikia tulipofika. Hakika wale wote waliohusika wanapaswa kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria za nchi.

8. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa nitaeleza hali halisi ya utekelezaji wa majukumu ya kazi mbalimbali za Wizara yangu katika kipindi cha mwaka wa fedha 2003/2004.

UTEKELEZAJI WA KAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2003/2004

9. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu katika kipindi cha fedha cha mwaka 2003/2004 imeendelea kupitia Ilani ya uchaguzi Mkuu ya CCM ya mwaka 2000, Dira ya 2020 ya Zanzibar na utekelezaji wa Mpango wa Kuondoa Umaskini, kuistawisha na kuiimarisha misingi ya Utawala Bora. Kufanikiwa kwa kazi hiyo mbali ya kuipa heshima Zanzibar pia itarahisisha upatikanaji wa maendeleo.

10. Mheshimiwa Spika, juhudi za kuleta maendeleo hazitaweza kuzaa matunda pasi na kuimarika kwa kiwango cha utawala bora tokea taasisi za Serikali, kibinafsi, vyama vya siasa, taasisi za kijamii na mtu mmoja mmoja. Kwa maana hiyo kazi ya uimarishaji wa Utawala Bora ni kazi inayoendelea na sisi sote tuna sehemu na wajibu katika hilo.

11. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2003/2004 Wizara yangu imeendelea vyema katika kuijenga misingi ya utawala bora kwa kazi ya kuelimisha umma kupitia programu ya elimu ya uraia, kuandaa sheria zenye

kuzipa uwezo taasisi mbalimbali ili ziweze kutekeleza majukumu yake kisheria. Aidha wadau wakuu mbalimbali wa Utawala Bora wameweza kunufaika kufuatia utekelezaji wa Mpango wa miaka mitano wa Utawala Bora wa Zanzibar chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa (UNDP). Katika kuimarisha sekta nzima ya Utawala Bora, Wizara yangu imepitisha pendekezo la uanzishwaji wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Kusimamia Maadili ya Viongozi na pendekezo la kuanzishwa kwa Idara ya Kuratibu Shughuli za Utawala Bora.

12. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha fedha 2003/2004 Idara ya Mahkama imeendelea kufanya kazi zake kwa kupokea kesi za jinai elfu tisa mia mbili na ishirini na mbili (9,222) na kuzitolea maamuzi elfu tano na arubaini na sita (5,046) na ilipokea kesi elfu moja mia tano na sabiini (1,570)za madai na kuzitolea maamuzi mia tano na hamsini na sita(556**) (Kiambatanisho A1).**

13. Mheshimiwa Spika, utoaji wa vipindi vya elimu ya uraia na shughuli za kidini zinaendelea kushughulikiwa na vyombo husika. Kazi za uandikishwaji wa vizazi na vifo pamoja na nyaraka mbalimbali nayo imeendelea ambapo jumla ya vizazi thalathini na sita elfu mia moja na hamsini na tisa (36,159) viliandikishwa **(Kiambatisho MM2)**.

14. Mheshimiwa Spika, katika kukuza ushirikiano na nchi mbalimbali, Wizara yangu katika kipindi cha mwaka 2003/2004 imeweza kupokea wageni na kubadilishana nao mawazo ya kikazi. Wageni hao wameonana na viongozi mbalimbali wa Wizara yangu. Aidha viongozi na wafanyakazi mbalimbali wamefanya ziara za nje katika kudumisha mashirikiano na maarifa ya kazi. Miongoni mwao ni ziara ya Waziri na ujumbe wake aliyoifanya katika nchi za Afrika ya Magharibi.

15. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004 Wizara yangu imeendelea na jukumu lake la ukusanyaji wa mapato ya Serikali kupitia zile taasisi zake zenye vyanzo vya mapato. Katika kipindi cha hadi mwezi wa Machi 2004 Wizara imeweza kukusanya jumla ya Shilingi milioni themanini na tisa laki tatu na sabiini na nane elfu mia nane na kumi na moja(89,378,811) kati ya lengo la Shilingi milioni mia moja na themanini na mbili laki tisa na hamsini na tano elfu (182,955,000.) Makusanyo hayo ni sawa na asilimia arobaini na nane nukta nane tano(48.85%) ya lengo.

16. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi, Wizara yangu ilikadiriwa kutumia jumla ya Shilingi bilioni tatu, mia moja na thalathini na tatu milioni,laki tatu na kumi na sita elfu (3,133,316,000)kwa kazi za kawaida na Shilingi milioni hamsini na mbili na arobaini elfu (52,040,000) kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2004 jumla ya Shilingi bilioni moja,mia tano na arobaini na tisa milioni,thelathini na sita elfu ,mia saba na thelethini ina mbili (1,549,036,732) zimepatikana kwa matumizi ya kazi za kawaida ikiwa ni sawa na asilimia arobaini na tisa nukta nne nne(49.44%) ya makadirio. Kati ya hizo jumla ya Shilingi bilioni moja , mia mbili na tisini na mbili , milioni laki nne na sabiini na nane elfu, mia tisa na tisini na tisa (1,292,478,999) zimetumika kwa ajili ya mishahara na maposho kwa wafanyakazi. Kwa upande wa kazi za maendeleo, jumla ya Shilingi kumi na nne milioni na laki saba (14,700,000) zimepatikana ikiwa ni sawa na asilimia ishirini na nane nukta mbili nne (**28.24%)** ya makadirio **[ufafanuzi zaidi kiambatanisho A3 (i), A3 (ii) na A3 (iii)].**

17. Mheshimiwa Spika, katika kuwaendeleza wafanyakazi kitaaluma jumla ya wafanyakazi mia moja na sitini na tano(165) wa kada mbalimbali wamepatiwa mafunzo ndani na nje; ya muda mrefu na mfupi. Kati ya hao wanawake ni sitini na saba (67) na wanaume ni tisini na nane(98.)Jumla ya wafanyakazi wapya thelathini na tisa(39) wameajiriwa ambapo wanawake ni ishirini na moja (21) na wanaume kumi na nane (18) **[kwa ufafanuzi zaidi angalia kiambatisho A2 (i), (ii)].**

18. Mheshimiwa Spika, utendaji niliioueleza ni wa kijumla tu na kwa vile kuna taasisi nyingi ndani ya Wizara yangu ni vyema kuueleza utekelezaji huo kupitia taasisi moja moja pale nitakapokuwa natoa maelezo ya kila taasisi.

MUUNDO WA WIZARA YA NCHI (AR) KATIBA NA UTAWALA BORA

19. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora ina jumla ya Taasisi kumi na mbili (12 **)** zifuatazo;

1. Idara ya Utawala na Uendeshaji
2. Idara ya Mahkama
3. Idara ya Mwanasheria Mkuu
4. Idara ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
5. Idara ya Mrajis Mkuu wa Serikali
6. Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana
7. Idara ya Mufti wa Zanzibar

8. Idara ya Mkurugenzi wa Mashtaka (Director of Public Prosecutions – DPP)
9. Taasisi ya Kuchunguza Maadili ya Viongozi
10. Taasisi ya Kupambana na Rushwa
11. Taasisi ya kusimamia Haki za Binaadamu
12. Afisi Kuu Pemba.

20. Mheshimiwa Spika, matarajio ya sasa ni kuwa na mabadiliko kutokana na dhamira ya kuunganisha Taasisi ya Kupambana na Rushwa na ile ya Kusimamia Maadili ya Viongozi kuunda mamlaka moja. Pia tunatarajia kuunda Idara ya Uratibu wa Shughuli za Utawala Bora, ambayo itahusisha pia masuala ya Haki za Binaadamu. Mabadiliko hayo yatafanya Wizara yangu iwe na jumla ya Taasisi kumi na moja(11**.)**

21. Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo ya Taasisi zilizomo ndani ya Wizara yangu kuna haja ya kujua utendaji wa taasisi hizo katika kipindi cha 2003/2004 kwa wajumbe na kwa wananchi kwa ujumla. Sasa naomba nitoe maelezo hayo sambamba na matatizo yaliyojitokeza, malengo na makadirio ya matumizi na mapato kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005.

IDARA YA UTAWALA NA UENDESHAJI

22. Mheshimiwa Spika, Idara ya Utawala na Uendeshaji katika kipindi cha 2003/2004 imeendelea kutekeleza vyema malengo na majukumu yake iliyojiwekea, huku pia ikiwa ni kiungo muhimu cha kuratibu kazi za Wizara. Utekelezaji wa kazi ulifanyika kupitia vitengo vyake mbalimbali kama ifuatavyo:-

Kitengo cha Elimu ya Uraia

23. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2003/2004 Idara kupitia kitengo hiki imeanza kazi ya utoaji wa vipindi vya Elimu ya Uraia kupitia Sauti ya Tanzania Zanzibar. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2004 jumla ya vipindi kumi na mbili (**12)** vilitolewa. Vipindi hivi vinatolewa siku ya Jumanne saa 1.30 usiku na kurudiwa siku ya Jumamosi saa 3.45 usiku. Aidha kitengo kimeandaa semina na kutoa taaluma kwa wasimamizi wa utawala bora ("Focal person") wa Wizara zote za Zanzibar na wadau Wakuu wa Utawala Bora. Azma ya semina hiyo ni kuwaelimisha wanasemina juu ya umuhimu wa mashirikiano ya kuimarisha misingi ya utawala bora ndani ya taasisi zao. Kitengo bado kinaendelea na kazi ya kuweka mkakati juu ya aina nyengine

mbalimbali zitakazotumika kutoa elimu ya uraia, maeneo mengine yanayotazamiwa ni kupitia televisheni, magazeti na vijarida.

Kitengo cha Kuratibu Jumuiya zisizo za Kiserikali

24. Mheshimiwa Spika, kitengo cha Kuratibu Jumuiya zisizo za kiserikali kimeweza kutekeleza kazi zake za kawaida kwa kiwango cha kuridhisha. Aidha kazi ya ukamilishaji wa matayarisho ya Sera ya Jumuiya imeendelea kwa hatua za kumuajiri mtaalamu. Baada ya mtaalamu kuipitia rasimu ya sera hiyo na kutoa mapendekezo, mkutano Mkuu wa wadau kutoka Serikalini, jumuiya zisizo za kiserikali na wafadhili ulifanyika kuichangia. Kazi inayoendelea sasa ni kwa mtaalamu kuzingatia mapendekezo ya wadau na baadae Wizara kufanya taratibu za kuwasilisha rasmi rasimu ya sera hiyo serikalini kwa hatua za ukamilishaji wake.

Kitengo cha Mipango, Utafiti na "Management Information System"

25. Mheshimiwa Spika, kama nilivyoahidi katika bajeti yangu ya mwaka jana kwamba Wizara yangu kwa mashirikiano na Shirika la Maendeleo la Kimataifa (UNDP) itatekeleza sehemu ya mapendekezo ya mpango wa Utawala Bora wa Zanzibar. Katika utekelezaji wa mpango huo hadi kufikia mwezi wa Machi 2004 Wadau Wakuu mbalimbali wa Utawala Bora wamenufaika. Miongoni mwao ni Idara ya Mahkama, Idara ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Tume ya Uchaguzi, Afisi ya Mwanasheria Mkuu, Jumuiya zisizo za kiserikali, Afisi ya Baraza la Wawakilishi, Wizara ya Vijana, Ajira, Maendeleo ya Wanawake na Watoto, Idara ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Afisi ya Mufti, n.k.

26. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ikiwa ndie msimamizi mkuu wa Sekta ya Utawala Bora, imefanya uratibu kwa kufanya mikutano na wadau wa Utawala Bora kujadili mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuanza jitihada za kutayarisha viashiria vya Utawala Bora. Vile vile Wizara imekuwa ikipokea fedha kutoka kwa wafadhili UNDP na kuwafikishia wadau wanaotekeleza miradi ya Utawala Bora walioko katika taasisi za Serikali na zile zisizo za kiserikali. Mambo makuu yaliyotekelezwa katika mpango huo ni pamoja na kujenga uwezo wa taasisi hizo kwa kutoa mafunzo kwa wafanyakazi, kuzipatia vifaa kama kompyuta, fotokopi, vipando na kuimarisha mawasiliano ya ndani na nje kupitia "Local Area Network" na pia "Internet". Aidha ushauri wa kitaalamu umetolewa katika kuzipa uwezo taasisi hizo kiuwajibikaji hali ambayo ilipelekea kuajiri washauri kwa muda.

27. Mheshimiwa Spika, kitengo katika kipindi cha 2003/2004 kimeratibu vyema vikao vya Kamati ya Uongozi kwa mujibu wa sheria. Aidha kimeongeza huduma ya "internet" kutoka moja hadi tatu na kukuza mtandao wa "Local Area Network" katika sehemu ambazo zilikuwa awali hazijafikiwa na huduma hiyo.

28. Mheshimiwa Spika, uanzishaji wa Kitengo cha Kuratibu Shughuli za Utawala Bora uko katika hatua za mwisho. Uchambuzi wa kina wa kazi zake umefanyika sambamba na uchambuzi wa kazi za taasisi mbalimbali za Wizara. Wizara imesharidhia mapendekezo ya uchambuzi huo na imeshatayarisha waraka wa kumalizwa suala hili Serikalini.

29. Mheshimiwa Spika, kazi za matengenezo ya jengo nazo zimeendelea katika kipindi cha mwaka 2003/2004. Wakati kazi za matengenezo ya jengo zikiendelea, Wizara imepata pigo la kuangukiwa na banda la kuegeshea gari. Banda hilo lilikuwa na uwezo wa kuegesha gari tano na lina gharama ya Shilingi milioni moja ,laki sita na thamanini na tisa elfu(1,689,000) kulingana na makisio yaliyotolewa na Idara ya Majenzi.

Kitengo cha Utumishi, Mafunzo na Maendeleo ya Wafanyakazi

30. Mheshimiwa Spika, kitengo hiki katika kipindi cha 2003/2004 kimeendelea kusimamia haki na wajibu wa wafanyakazi. Aidha nidhamu na maendeleo yao yamesimamiwa vyema. Katika kipindi hicho kitengo kimeweza kusimamia mafunzo ya wafanyakazi thalathini na nne (34) . Kati ya hao wanawake ni kumi na tano (15) na wanaume ni kumi na tisa (19). Miongoni mwao tisa (9) wanahudhuria mafunzo ya muda mrefu na wengine ama wamepata au wanaendelea na mafunzo ya muda mfupi. Mafunzo waliyoyapata yanahusu zaidi maeneo ya Sheria, Uhasibu, Uchumi, Utawala Bora, Kompyuta, Ukarani n.k. Pia kitengo kimeendelea kuwasimamia wafanyakazi saba (7) ambao wanaendelea na masomo ya muda mrefu tokea miaka ya nyuma **[ufafanuzi zaidi kiambatanisho A4(i) na A4(ii)].**

31. Mheshimiwa Spika, mbali na mafanikio yaliyopatikana, Idara ya Utawala na Uendeshaji katika kipindi cha 2003/2004 ilikabiliwa na matatizo yafuatayo:-

(i) uhaba wa nyenzo za kufanyia kazi;

(ii) uhaba na uchakavu wa vyombo vya usafiri;

(iii) uhaba wa wataalamu; na

(iv) uhaba wa nafasi za afisi za kufanyia kazi.

32. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005 Idara ya Utawala na Uendeshaji imejipangia malengo yafuatayo:-

(i) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa mapendekezo ya Mpango wa Utawala Bora wa Zanzibar; na kuendelea na jitihada za kupitishwa kwa mpango huo kama Waraka wa Serikali.

(ii) kuwaendeleza wafanyakazi kitaaluma;

(iii) kuendelea na kazi ya kuratibu shughuli za Wizara;

(iv) kuendelea na kazi ya matengenezo ya jengo;

(v) kuandaa Mpango wa Kimkakati wa Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora; na

(vi) kuimarisha shughuli za kimahesabu kwa kuingia katika mfumo wa matumizi ya kompyuta (Computerization of the Accounting System).

33. Mheshimiwa Spika, ili Idara ya Utawala na Uendeshaji iweze kutekeleza malengo yake katika kipindi cha fedha cha 2004/2005 naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi mia tano na kumi na nane milioni,laki mbili na thalathini na nne elfu (518,234,000) kwa kazi za kawaida na Shilingi milioni ishirini ,laki nane na arobaini elfu (20,840,000) kwa kazi za maendeleo.

KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA

34. Mheshimiwa Spika, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana katika kipindi cha 2003/2004 imeendelea kutekeleza majukumu yake kama ilivyojipangia kupitia vitengo vyake kama ifuatavyo:

Kitengo cha Urithi

35. Mheshimiwa Spika, kupitia kitengo cha urithi, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, imeweza kutoa taaluma ya sheria ya Mirathi kwa wananchi.

Aidha Kamisheni imeweza kutatua migogoro mingi ya mirathi baina ya wanafamilia wa Kiislamu. Migogoro minane imepatiwa ufumbuzi kupitia Mahkama kabla ya hatua ya urithi. Jumla ya tirka mia tatu na thalathini na nane (338) zimefunguliwa na tirka kongwe mia moja na ishirini na mbili (122) zenye thamani ya Shilingi milioni mia tatu na kumi,laki saba na sabiini na mbili elfu,mia tatu na sabiini na tatu (310,772,373) zimefungwa.

Kitengo cha Wakf

36. Mheshimiwa Spika, kupitia kitengo cha Wakfu, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana katika kipindi cha 2003/2004 imeweza kuzitunza jumla ya nyumba mia nne na sabiini na sita (476), kati ya hizo tisiini na moja (91) za Amana ambapo Unguja zipo sabiini(70) na Pemba ishirini na moja(21). Aidha kitengo kimekusanya jumla ya Shilingi milioni hamsini na sita,laki moja na arobaini na tatu elfu na mia moja (56,143,100) kutokana na kodi za nyumba za Wakfu, Shilingi milioni nane laki saba na arobaini na moja elfu (8,741,000) kodi za nyumba za Amana ziliopo Unguja na Shilingi milioni mbili,laki tano na hamsini na mbili elfu mia tatu na thalathini na tatu na senti thalathini (2,552,333.30) kutokana na kodi ya nyumba hizo ziliopo Pemba. Kwa upande wa Mashamba Kamisheni imeweza kuendelea kuvitunza jumla ya vikataa kumi na mbili(12) na shamba moja. Mapato kwa vikataa na shamba yalikuwa Shilingi laki nne na tisini na nane elfu (498,000).

37. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi wa Machi 2004 kitengo kiliweza kukusanya Shilingi milioni sitini na saba,laki tisa na thalathini na na nne elfu,mia nne na thalathini na tatu (67,934,433) sawa na asilimi tisini na saba(97) ya lengo. Matarajio ni kuvuka lengo lililowekwa la Shilingi milioni sabiini (70,000,000) hadi tarehe ya leo. Jumla ya Shilingi milioni kumi na sita,laki saba na ishirini na sita elfu,mia saba na hamsini na tano(16,726,755)zilitumika katika kufanyia matengenezo madogo madogo kwa nyumba kumi na tisa (19.)

Kitengo cha Shughuli za Kiislamu

38. Mheshimiwa Spika, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kupitia kitengo cha Shughuli za Kiislamu imeweza kusimamia vyema Sala na Mabaraza ya Iddi pamoja na shughuli mbalimbali za kidini na kijamii zinazohusu dini ya Kiislamu. Miongoni mwao ni pamoja na kurahisisha upatikanaji wa Wafadhili wa kusaidia katika mambo ya Zakka, Sadaka na Misaada ya Kiislamu.

39. Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka uliopita niliahidi kuwa Wizara itaangalia uwezekano wa kuifanya Kamisheni kubakia kama mratibu wa Safari za Hijja na kuondokana na kujihusisha moja kwa moja na upelekaji wa mahujaji. Napenda kulijulisha Baraza hili tukufu kuwa hatua hii imetekelezwa.

40. Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuzishukuru taasisi binafsi zilizosafirisha Mahujaji kama ifuatavyo: *Zanzibar Istiqama Hajj and Travelling Agency* iliyosafirisha Mahujaji mia moja na arubaini na tano(145), *Jumuiya ya Istiqama Tanzania mia moja na ishirini na nne* (124), *Khidmat Islamiyya Charitable Society arubaini* (40) *Zanzibar Hajj Travelling Agency arubaini na saba* (47) na *Ahlu Daawa ishirini na mbili* (22). Pamoja na kuratibu misafara hii, Kamisheni iliweza kusimamia misafara miwili (2), mmoja ukiwa ni ule wa Mheshimiwa Rais ishirini na mbili (22) na ule wa Mufti kumi na sita (16). Mahujaji hawa ni mia nne na kumi na sita(416) kati ya Mahujaji mia tisa na thalathini na sita(936) wa Tanzania nzima.

41. Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kuona umuhimu wa Wizara kupitia Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kutojitoa moja kwa moja kwenye shughuli za Hijja. Wizara imeafiki hilo kwa kuwa Kamisheni bado ni tegemeo kubwa kwa vikundi vyetu vichanga vinavyopeleka Mahujaji. Tunaamini pia kuwa hili haliizuii Kamisheni kupeleka Mahujaji pale itakapokuwa na uwezo wa kufanya hivyo.

Kitengo cha Mahusiano

42. Mheshimiwa Spika, Kamisheni kupitia kitengo chake cha Mahusiano katika mwaka 2003/2004 kimeendelea na kazi ya kujenga mahusiano mema kati ya Kamisheni na watu binafsi, taasisi za ndani na nje ya nchi. Katika kipindi cha Julai 2003 hadi March 2004 kitengo kimeweza kufanikisha semina sita (6) katika Wilaya nne za Unguja na mbili za Pemba zilizoshirikisha Masheha na Makatibu wao. Semina hizo pamoja na mambo mengine ziliwabainishia Masheha majukumu yao kuhusiana na mas-ala ya Mirathi na Nyakfu. Pia kimekuwa kikikusanya na kutoa taarifa mbalimbali muhimu za utendaji wa Kamisheni, kutoa ushauri na taaluma kwa watendaji wa Kamisheni na wateja wengine na kuendeleza mashirikiano na taasisi mbalimbali za Kidini hapa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Kitengo cha Utawala na Utumishi

43. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu bado inalishughulikia tatizo la afisi Kisiwani Pemba. Itakumbukwa kuwa Kamisheni ya Wakf na Mali ya Amana inacho kiwanja katika mji wa Wete ambacho kimeshaanza kuendelezwa. Hata hivyo, juhudi za kukiendeleza kiwanja hicho zimekwama kwa ukosefu wa fedha. Kwa kuona umuhimu wa kuwa na afisi inayolingana na hadhi ya Kamisheni, alitafutwa mfadhili wa kusaidia ujenzi huo ambapo Ali Yusuf Charitable Society ilikubali kusaidia. Baada ya kukikagua kiwanja hicho, mfadhili huyo alibadilisha uamuzi na kupendekeza Afisi hiyo ijengwe katika mji wa Chake Chake.

44. Mheshimiwa Spika, kiwanja kwa ajili ya kujenga Afisi hiyo Chake Chake kimepatikana na ni matumaini ya Wizara kwamba mfadhili huyo atatimiza ahadi yake. Kwa kuzingatia kwamba kiwanja cha Wete kimeshaanza kuendelezwa, Wizara itaendeleza juhudi hizo kidogo kidogo kulingana na upatikanaji wa fedha.

45. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kuwaendeleza wafanyakazi kitaaluma, hadi kufikia mwezi wa Machi 2004 jumla ya wafanyakazi watatu(3) wamepatiwa masomo, kati ya hao wawili(2) wanahudhuria masomo ya muda mrefu na mmoja(1) anahudhuria masomo ya muda mfupi. Kamisheni bado inawaendeleza vijana watatu (3) ambao wanaendelea na masomo.

46. Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo Kamisheni katika kipindi cha 2003/2004 imekabiliwa na matatizo yafuatayo:

(i) uhaba wa nafasi katika afisi zake;

(ii) ugumu wa kiutendaji unaotokana na mapungufu yaliyopo katika Sheria Namba 5 ya 1980; na

(iii) ugumu wa kupata malipo ya deni la Shilingi milioni thanini na nane,laki tisathalathini na nane elfu na mia mbili (88,938,200)zinazodaiwa taasisi mbalimbali za Serikali.

47. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005 Kamisheni imejiwekea malengo yafuatayo:-

(i) kuendelea kutekeleza wajibu wake kulingana na Sheria namba 5 ya 1980;

(ii) kuendelea na kazi za kutoa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria namba 5 ya l980 na muundo wa Kamisheni na kuona kwamba kazi hiyo inakamilika;

(iii) kuwaendeleza wafanyakazi wake; na

(iv) kufuatilia madeni ya Kamisheni.

48. Mheshimiwa Spika ili Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana iweze kumudu vyema kutekeleza majukumu na malengo iliyojiwekea katika kipindi cha mwaka 2004/2005 ninaliomba Baraza lako tukufu liidhinishe ruzuku ya Shilingi milioni mia moja naishirini na tano,laki nne na tisini na moja elfu (125,491,000) Kwa ajili ya kukimu matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA MAHKAMA

49. Mheshimiwa Spika, Idara ya Mahkama katika kipindi cha 2003/2004 imeendelea vyema na kazi zake kwa mujibu wa Katiba na Malengo iliyojipangia. Kazi za Idara hii zinafanywa ikiwa ni moja ya mihimili mitatu ya Dola. Utekelezaji wa majukumu umezihusisha sehemu na vitengo mbalimbali kama ifuatavyo:-

Kitengo cha Utawala na Uendeshaji

50. Mheshimiwa Spika, kupitia kitengo hiki, Idara ya Mahkama kwa mashirikiano na Afisi ya Mwanasheria Mkuu imeweza kuandaa Rasimu ya Mswada wa Sheria ya Tume ya Utumishi ya Mahkama. Rasimu hiyo ilipitishwa na Baraza lako tukufu katika kikao cha mwezi Oktoba 2003. Kukamilika kwa Sheria hiyo ni hatua muhimu katika kuimarisha Misingi ya Utawala Bora, kwani kunatoa nafasi ya kuwachukulia hatua za kinidhamu maafisa mbalimbali wa Mahkama ambao watakwenda kinyume na maadili ya kazi. Aidha kunaleta faraja kwa watendaji juu ya uwezo wa kushughulikia maslahi ya maafisa wa Idara ya Mahkama.

51. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha hadi mwezi wa Machi 2004 Idara ya Mahkama imewapeleka masomoni wafanyakazi arubaini (40) ndani na nje ya Nchi. Kati yao mfanyakazi mmoja (1) anasomea Digrii ya Kwanza ya Sheria, wawili wanasomea Diploma ya Sheria na wafanyakazi thalathini na saba (37) wamepatiwa mfunzo ya muda mfupi ya kompyuta. Kati ya hao wanawake kumi na tisa(19) na wanaume ishirini na moja (21). Masomo hayo yanawahusisha Mahakimu na Makarani. Pia Idara inaendelea kutafuta nafasi

zaidi za masomo kwa wafanyakazi wake katika maeneo mengine ili kuendelea kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

52. Mheshimiwa Spika, kupitia kitengo hicho kwa mwaka 2003/2004 jumla ya Mahakimu wanne wa Mkoa waliajiriwa, ambapo wanawake ni watatu na tayari wameanza kazi katika Mikoa ya Unguja na Pemba. Hii imepunguza tatizo la uhaba wa Mahakimu katika mikoa yetu. Vile vile kila Mkoa wa Unguja na Pemba kumeanzishwa Mahakama ya Mkoa na kupangiwa Mahakimu. Ni matumaini yetu kuwa tatizo la Mahakimu wa Mkoa litakwisha kabisa baada ya watumishi wa Idara hii kumaliza masomo yao ndani ya miaka miwili kuanzia sasa.

53. Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha unaomalizika Idara ya Mahkama kwa mashirikiano na Mahkama ya Rufaa ya Tanzania na kwa msaada wa European Commission iliandaa Semina ya siku mbili ya Majaji Wakuu wa Nchi za **SADC** iliyofanyika hapa Zanzibar. Aidha Mkutano wa Majaji wa Nchi za Afrika ya Mashariki nao ulifanyika hapa Zanzibar mwezi Oktoba, 2003

54. Mheshimiwa Spika, Idara ya Mahkama imeendelea kuyafanyia matengenezo majengo yake Unguja na Pemba. Hata hivyo kutokana na ukosefu wa fedha, kasi ya matengenezo hayo haikwenda kama ilivyotarajiwa, lakini UNDP imeisaidia Idara ya Mahkama katika kukabiliana na tatizo hilo, kwa kugharamia fedha za kutathmini hali ya majengo ya Mahkama na kuinua elimu ya watumishi wa vyombo vya sheria. Kazi hiyo iligharimu Shilingi milioni thalathini na mbili,thamanini na tatu elfu na thalathini (32,083,030). Aidha Shirika hilo kupitia Tume ya Rais ya Pamoja ya Muafaka wamekabidhi vitabu mbalimbali vya Sheria kwa ajili ya matumizi ya Maktaba ya Mahkama Kuu.

55. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004 Idara ya Mahkama imeendelea na kazi yake ya utoaji wa huduma ya kusikiliza kesi katika ngazi zake mbalimbali. Usikilizaji huu wa kesi unahusisha kesi za jinai na madai. Aidha mashauri ya Sheria ya Kiislam yalishughulikiwa na Mahkama ya Kadhi. Kwa ujumla hali ilikuwa kama ifuatavyo:-

Mahkama ya Mwanzo

56. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwezi wa Machi 2003 hadi kufikia Februari 2004 Mahkama ya Mwanzo imeweza kupokea jumla ya kesi elfu tatu mia moja na sitini na moja(3,161) za jinai ikiwa ni ongezeko la asilimia sita (6) ya kesi zilizopokelewa mwaka uliopita, kati ya hizo kesi elfu

moja mia nane na hamsini na saba(1,857) zimetolewa uamuzi na kesi elfu moja mia tatu na nne(1304) zinaendelea. Aidha Mahkama hii imepokea kesi mia tatu na ishirini na nane (328) za madai ikiwa ni ongezeko la asilimia moja(1) ya kesi za aina hii zilizopokelewa mwaka uliopita. Kesi mia moja na tatu (103) zimetolewa uamuzi na mia mbili na ishirini na na tano(225) zinaendelea.

Mahkama ya Wilaya

57. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi wa Februari 2004 Mahkama ya Wilaya imepokea jumla ya kesi elfu tano mia mbili na sitini na nne(5,264)za jinai ikiwa ni pungufu kwa asilimia nne nukta mbili(4.2) kulinganisha na mwaka uliopita. Kesi elfu tatu na sitini na tisa (3,069) zimetolewa uamuzi na kesi elfu mbili mia moja na tisini na tano (2,195) bado zinaendelea. Aidha jumla ya kesi mia tatu na thalathini na tisa (339) za madai zimepokelewa na kati ya hizo arubaini na nane(48) zimetolewa uamuzi na kesi mia mbili na tisini na moja (291) bado zinaendelea. Pia rufaa sita (6) za jinai zimefunguliwa na tatu (3) kutolewa uamuzi na tatu (3) bado zinaendelea. Kwa upande wa madai rufaa kumi na moja (11) zilifunguliwa, 5 zilitolewa uamuzi na 6 zinaendelea.

Mahkama ya Mkoa

58. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2003/2004 jumla ya kesi mia sita na ishirini na mbili (622) za jinai zimepokelewa ikiwa ni ongezeko la asilimia zero nukta sita (0.6) kwa kulinganisha na kesi zilizopokelewa katika Mahkama hii katika kipindi kama hicho mwaka uliopita. Kati ya hizo kesi thamanini na sita (86) zimetolewa uamuzi na kesi mia tano na thalathini na sita(536) zinaendelea. Kwa upande wa kesi za madai zilizopokelewa ni mia moja na ishirini na na tisa(129) na kati ya hizo kumi na tatu (13) zimetolewa uamuzi na mia moja kumi na sita (116) bado zinaendelea. Rufaa arubaini na nne (44) za jinai zimefunguliwa kumi na nne (14) zimetolewa uamuzi thalathini (30) bado zinaendelea. Aidha kesi arubaini na nne (44) za rufaa ya madai zilifunguliwa kati ya hizo tano (5) zimetolewa uamuzi na thalathini na tisa (39) zinaendelea.

Mahkama Kuu

59. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2003/2004 Mahkama Kuu ilipokea jumla ya kesi za jinai ishirini na tatu (23) ambazo kati ya hizo sita (5) zimetolewa uamuzi na kumi na nane(18)bado zinaendelea. Kwa upande wa kesi za madai, Mahkama hiyo ilipokea kesi sitiini na moja (61) na tayari kumi na tano(15) zimetolewa uamuzi na kesi arubaini na sita(46) zinaendelea.

Kuhusu rufaa za madai Mahkama ilipokea kesi sitini na sita(66) na kati ya hizo kumi na tisa(19) zimetolewa uamuzi na arubaini na saba(47) zinaendelea. Kesi za Probate mia moja na ishirini na saba (127) zilipokelewa, tisiini na mbili(92) zimetolewa uamuzi na thalathinin na tano(35) zinaendelea.

60. Mheshimiwa Spika, Mahkama ya Rufaa ilifanya kikao cha kusikiliza kesi za Zanzibar kuanzia tarehe 15 Oktoba, hadi 21 Novemba, 2003 ambapo jumla ya kesi hamsini na mbili(52) zilisikilizwa. Kesi tatu(3) kati ya hizo zilikuwa ni za rufaa ya jinai kutokana na uamuzi wa Mahkama Kuu ambazo zote zilisikilizwa na kutolewa uamuzi. Aidha ombi moja la jinai (Criminal Application) lilisikilizwa na kutolewa uamuzi. Mahkama hiyo pia ilisikiliza rufaa thalathini na moja(31) za madai (Civil Appeals) ambapo rufaa ishirini na mbili (22) kati ya hizo zilitolewa uamuzi na rufaa tisa(9) zimeahirishwa hadi katika kikao kinachotegemewa kufanyika Zanzibar mwezi wa Septemba 2004. Vile vile maombi ya madai kumi na saba (17) (Civil Applications) yalisikilizwa kumi na mbili(12) yalitolewa uamuzi na matano yameahirishwa hadi kikao cha mwaka huu.

Mahkama ya Kadhi

61. Mheshimiwa Spika, hadi Febuari 2004 Mahkama ya Kadhi imepokea jumla ya kesi mia saba na kumi na tatu(713) katika ngazi ya Wilaya ikiwa ni ongezeko la asilimia zero nukta saba(0.7) ya ile idadi ya kesi zilizofunguliwa katika kipindi kama hicho cha mwaka uliopita. Kati ya hizo kesi mia tatu na sabiini na saba (377) zimetolewa uamuzi na mia tatu na thalathini na sita (336) zinaendelea kusikilizwa. Mahkama ya Kadhi wa Rufaa imepokea rufaa thalathini na tisa(39) ikiwa ni pungufu kwa asilimia zero nukta tatu (0.3) ya kesi zilizopokelewa katika kipindi kama hiki mwaka uliopita. Kati ya kesi hizo ishirini na tano(25) au asilimia sabiini na tano(75) zimeweza kutolewa uamuzi.

Mahkama ya Watoto

62. Mheshimiwa Spika, hadi Febuari 2004 Mahkama ya watoto imepokea jumla ya kesi za jinai mia moja na hamsini na mbili(152). Hii ni sawa na ongezeko la asilimi zero nukta(0.7) ya kesi zilizopokelewa katika kipindi kama hicho mwaka uliopita. Kati ya kesi hizo ishirini na tisa(29) zimetolewa uamuzi na mia mojaj na ishirini na tatu(123) zinaendelea.

63. Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio iliyopata Idara ya Mahkama katika kipindi cha 2003/2004 bado imekabiliwa na matatizo yafuatayo:-

(i) uchakavu wa majengo ya Mahkama ;

(ii) ufinyu na Uhaba wa vyumba vya kusikilizia kesi ;

(iii) upungufu wa vitendea kazi; na

(iv) kurundikana kwa kesi ambako kunachangiwa na ukosefu wa vitendea kazi pamoja na kushindwa kukamilisha upelelezi kwa polisi.

64. Mheshimiwa Spika, Idara ya Mahkama hadi kufikia mwezi wa Febuari, 2004 imeweza kukusanya jumla ya Shiling milioni kumi na saba,laki sita na hamsini na saba elfu,mia tisa na sabiini na tano(17,657,975) kati ya lengo lililowekwa la Shilingi milioni thalathini ,laki tano na elfu sita (30,506,000). Katika mwaka wa fedha 2004/2005 Idara imejiwekea lengo la kukusanya na kuchangia katika mfuko Mkuu wa Serikali jumla ya Shilingi milioni thalathini na moja(31,000,000/).

65. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005 Idara ya Mahkama imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

(i) kuendelea na kazi ya matengenezo ya majengo ya Mahkama kwa Unguja na Pemba na upatikanaji wa vitendea kazi;

(ii) kuandaa Semina kwa ajili ya wafanyakazi ili kuinua utendaji kazi kwa Idara ya Mahkama pamoja na wadau wa kesi za mahkama;

(iii) kuendelea na utoaji wa huduma ya usikilizaji na utoaji wa maamuzi katika kesi mbalimbali kupitia Mahkama zake; na

(iv) kuendelea na jitihada za kuwaendeleza wafanyakazi kielimu.

66. Mheshimiwa Spika, Ili Idara ya Mahkama iweze kutekeleza malengo yake iliyojipangia kwa mwaka wa 2004/2005 naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi milioni mia nane na hamsini (850,000,000) kwa kazi za kawaida**.**

IDARA YA MRAJIS MKUU WA SERIKALI

67. Mheshimiwa Spika, Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali katika kipindi cha 2003/2004 imeendelea vyema kutekeleza malengo iliyojipangia. Afisi imekamilisha kazi ya marekebisho ya Muundo wake wa Utumishi (Scheme of Service) na umeshawasilishwa Idara ya Utumishi kwa hatua zaidi.

68. Mheshimiwa Spika, Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali katika kipindi cha 2003/2004 imewaelimisha wamiliki wa Makampuni na Jumuiya zisizo za kiserikali juu ya wajibu wao kwa Taifa na umuhimu wa kufuata katiba zao. Afisi iliweza kutoa miongozo ya kikatiba katika jumuiya zaidi ya nane.

69. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2003/2004 Afisi imeweza kuwaendeleza wafanyakazi wake kitaaluma. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2004 jumla ya wafanyakazi saba wameanza kupatiwa mafunzo ya sheria. Kati ya hao wanaume wane(4) na wanawake ni watatu (3.) Vile vile wafanyakazi watatu wanaendelea na masomo. Aidha katika kuleta utendaji bora wa kazi, Afisi katika kipindi cha 2003/2004 imefanya marekebisho ya kanuni za Sheria ya Alama za Biashara kutoka madaraja ya kitaifa na kutumia ya kimataifa. Aidha mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya usajili wa alama za biashara yameshafanywa.

70. Mheshimiwa Spika, Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali katika kipindi cha 2003/2004 imefanikiwa kusimamia na hatimae kupitishwa kwa Sheria ya Hakimiliki na tayari imekamilika. Kupitishwa kwa sheria hii kutasaidia kulinda maslahi ya wasanii wetu pamoja na wavumbuzi mbalimbali. Aidha Afisi inatarajia kufanya semina kwa wadau ili kuamsha uelewa wao juu ya sheria hii. Vile vile katika kujiimarisha na utoaji wa huduma katika ulimwengu huu wa sayansi na teknologia, Afisi ya Mrajis imeshaalika makundi ya wataalamu wa Kompyuta kwa ajili ya kutathmini na kuandaa “Data base” ya Vizazi na Vifo. Jumla ya “Proposal documents” nne zimeshawasilishwa na kazi ya kuzifanyia uchambuzi inaendelea.

71. Mheshimiwa Spika, Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali katika kipindi cha 2003/2004 imefanikiwa kwa mashirikiano na Wizara ya Fedha na Uchumi kufanya semina kwa masheha na watendaji wengine wanaohusika na kazi za Afisi. Jumla ya Semina sita kwa Wilaya sita zimefanyika ambapo kwa Unguja zilihusika Wilaya za Kaskazini A, Kaskazini B, Kusini na Wilaya ya Kati. Kwa upande wa Pemba ni Wilaya za Mkoani na Chake chake. Mipango inaandaliwa kwa Wilaya zilizobaki.

72. Mheshimiwa Spika, Afisi ya Mrajis Mkuu katika kipindi cha 2003/2004 imeendelea na kazi zake za kawaida kama ifuatavyo:-

Kitengo cha Uandikishaji wa Vizazi, Vifo na Tirka za Mali-Maiti

73. Mheshimiwa Spika, Kitengo hiki katika kipindi cha mwaka 2003 kimeweza kusajili vizazi elfu thalathini na sita,mia moja na hamsini na tisa (36,159) kati yake vizazi elfu kumi na nane ,mia tano na sitini na tatu (18,563) ni vya watoto wanaume na elfu kumi na saba,mia tano na tisini na sita (17,596) ni wanawake. Idadi hii ni ongezeko la asilimia tatu(3) kulinganisha na usajili wa mwaka uliopita. Jumla ya vifo elfu nne mia tatu na thamanini na tatu(4,383) vimeandikishwa. Katika kipindi hicho hicho jumla ya tirka za mali-maiti kumi na mbili (12) ziliweza kushughulikiwa kwa wasio kuwa waislamu. Katika kipindi cha Januari hadi mwezi wa Machi 2004, jumla ya vizazi elfu nane,mia moja na thamanini na saba (8,187) vimeandikishwa na vifo mia nane kumi na saba(817) **(*ufafanuzi zaidi kiambatanisho MM2).***

Kitengo cha Usajili wa Makampuni.

74. Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Makampuni kimeendelea na kazi zake kama kawaida. Kwa mwaka 2003 makampuni tisiini na na sita (96) yamesajiliwa, miongoni mwa makampuni hayo sabiini na nane (78) ni makampuni ya hapa nchini na kumi na nane(18) ni makampuni ya kigeni. Idadi imepungua kwa asilimia kumi na saba (17) ikilinganishwa na makampuni mia moja kumi na tatu (113) yaliyosajiliwa mwaka 2002. Pia makampuni ishirini na nne(24) yamesajiliwa kwa kipindi cha mwezi Januari mpaka Machi mwaka 2004. Kwa upande wa Majina ya Biashara, jumla ya Majina ya Biashara mia moja kumi na nane(118) yamesajiliwa kwa kipindi cha mwaka 2003, na kwa kipindi cha mwezi Januari hadi Machi 2004 jumla ya Majina ya Biashara hamsini (50) yamesajiliwa ***(Ufafanuzi zaidi Kiambatisho MM3).***

Kitengo cha Usajili wa Mali za Ubunifu

75. Mheshimiwa Spika, Kitengo hiki kinashughulika na kazi za usajili wa mali za ubunifu *(Intellectual Property).* Kabla, kitengo hiki kilikuwa kinafanya usajili wa alama za biashara (*Trademarks)* na kazi za uvumbuzi *(Patents)* tu. Hata hivyo shughuli zote zinazohusiana na Hakimiliki zitasimamiwa na kitengo hiki. Jumla ya Alama 300 zimesajiliwa mwaka 2003, wakati Alama za biashara tisiini na tano(95) zimesajiliwa hadi kufikia mwezi wa Machi 2004. Mbali na usajili huo Afisi ya Mrajis imesajili alama za uvumbuzi ishirini na moja(21) kwa mwaka 2003, na kwa kipindi cha mwezi Januari hadi Machi

mwaka 2004 alama moja(1) tu ya uvumbuzi ndio iliyosajiliwa ***(Ufafanuzi zaidi Kiambatisho MM3).***

Kitengo cha Usajili wa Nyaraka.

76. Mheshimiwa Spika, Kitengo hiki kimeendelea na kazi za usajili wa nyaraka za aina mbalimbali. jumla ya nyaraka mia nane na arubaini na nane (848) zimesajiliwa mwaka 2003, hadi kufikia mwezi Machi mwaka huu, jumla ya nyaraka mia moja na hamsini na saba(157) zimesajiliwa Unguja na Pemba. Kitengo pia kina jukumu la kufanya usajili wa ndoa na talaka, ambapo kwa mwaka 2003 jumla ya ndoa thamanini(80) na talaka kumi na sita (15) zilisajiliwa. Na kwa kipindi cha mwezi Januari mpaka Machi 2004 jumla ya ndoa hamsini na saba(57) na talaka kumi na tano (15) zimesajiliwa ***(Ufafanuzi zaidi Kiambatisho MM4).***

Kitengo cha Usajili wa Jumuiya Zisizo za Kiserikali (NGO's na CBO's)

77. Mheshimiwa Spika, jukumu kubwa la kitengo hiki ni kufanya usajili pamoja na kuzifuatilia jumuiya zisizo za kiserikali zinazosajiliwa kwa kutumia Sheria namba 5 ya mwaka 1995. Kwa kipindi chote cha mwaka 2003 jumla ya Jumuiya arubaini na tatu (43) zilisajiliwa, ambapo Jumuiya 8 zimesajiliwa kwa kipindi cha mwezi Januari hadi Machi mwaka 2004. Idadi hii imeongezeka kwa zaidi ya asilimia sitini na tano(65) ikilinganishwa na ile ya mwaka 2001 ambapo Jumuiya arubaini na mbili(42) zilisajiliwa, **(Ufafanuzi zaidi Kiambatisho MM5).**

78. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapato jumla ya Shilingi milioni mia moja na kumi na saba ,laki saba na sabiini na tisa elfu,mia nane na thalathini na tatu na senti sabiini (117,779,833.70) zimekusanywa. Kati ya hizo Shilingi milioni arubaini na saba,hamsini na nane elfu ,mia tisa na tisiini na nane (47,058,998.00) zimeingia moja kwa moja kwenye mfuko wa Bodi ya Mapato, na Shilingi milioni sabiini,laki saba na ishirini elfu mia nane na thalathini na sita(70,720,836) zimeingia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Idadi hiyo ya fedha zilizokusanywa ni sawa na asilimia sabiini na nane (78) ya malengo iliyojiwekea. Kwa mwaka wa fedha 2004/2005, Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali inakusudia kukusanya na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali jumla ya Shilingi milioni mia moja na kumi na nne na arubaiini elfu (114,040,000) **(Ufafanuzi zaidi Kiambatisho MM1).**

79. Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada zote hizo zilizochukuliwa na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu yake, Afisi ya Mrajis

Mkuu wa Serikali inaendelea kukabiliwa na matatizo kadhaa. Miongoni mwa matatizo hayo ni :-

(i) ukosefu wa vifaa vya kisasa vya kuhifadhia kumbukumbu pamoja na uchakavu wa zana za kufanyia kazi ;

(ii) upungufu wa vifaa vya kuandikia (Stationaries) ikiwa ni pamoja na karatasi za kuandikia vyeti vya kuzaliwa, Mabuku ya B1, Mabuku ya ndoa na talaka, pamoja na fomu za maombi mbalimbali ya usajili ; na

(iii) uhaba na uchakavu wa vyombo vya usafiri .

80. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005 Afisi ya Mrajis Mkuu imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

(i) kuendelea na kazi za kutoa taaluma kwa wateja na watendaji wake wote wanaohusika na kazi za Afisi ya Mrajis hasa za usajili ;

(ii) kuwaendeleza wafanyakazi kitaaluma kwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi hasa katika fani ya sheria ;

(iii) kukamilisha kazi ya kuzipitia na kuzifanyia marekebisho sheria za Majina ya Biashara na Vizazi na Vifo, pamoja na kuzipitia sheria nyengine zinazoongoza kazi za Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali ;

(iv) kuanzisha mpango wa kusajili alama za biashara (“Trademark”) kwa kutumia kompyuta, na kutafuta fedha kwa ajili ya mradi wa kuandikisha Vizazi na Vifo kwa kutumia kompyuta kwa Wilaya zote za Zanzibar ;

(v) kuanzisha “Website” ya Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali ;

(vi) kununua zana za kisasa za kutendea kazi ; na

(vii) Kulifanyia matengenezo jengo la Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali la Unguja pamoja na kutafuta jengo jengine kwa ajili ya Afisi ya Mrajis huko Pemba.

81. Mheshimiwa Spika, ili Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali iweze kutekeleza malengo hayo iliojiwekea kwa mwaka wa fedha 2004/2005

naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi milioni mia mbili na sita,laki saba na elfu nane(206,708,000) kwa matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA MUFTI WA ZANZIBAR

82. Mheshimiwa Spika, Idara ya Mufti katika kipindi cha mwaka 2003/2004 iliendelea vyema kutekeleza malengo na majukumu yake kupitia vitengo vyake mbalimbali kwa mujibu wa Sheria namba 9 ya mwaka 2001.

83. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2003/2004 Idara imeshughulikia utoaji wa *FATWA* na utatuzi wa migogoro inayohusu au inayohitaji elimu ya dini ya Kiislamu. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2004 jumla ya migogoro thamanini na tatu(83) ilipokelewa na migogoro sabiini na tatu (73) ilipatiwa ufumbuzi. Masuali elfu moja mia moja na thalathini na tano (1135) yamepokelewa hadi kufikia mwezi wa Machi 2004. ikilinganishwa na masuali 950 yaliyopokelewa katika kipindi kama hicho mwaka 2003. Masuali mia nne na sitiini (460) kati ya elfu moja mia moja na thalathini na tano (1135) yamejibiwa.

84. Mheshimiwa Spika, Idara ya Mufti imekuwa ikiratibu vyema suala la kujenga mahusiano mema ndani na nje ya nchi. Kwa upande wa ndani, Idara imeweza kuratibu ziara za Mheshimiwa Mufti kwa kuitembelea misikiti kumi na nne(14.) Hatua hii inatoa fursa kati ya waumini na Afisi kubadilishana mawazo. Pamoja na hayo pia Afisi imewasiliana na jumuiya mbalimbali za Kiislamu hapa nchini, miongoni mwao ni Fiy Sabili-Llahi Tabligh Markaz, Woman Muslim Academy, Jumuiya ya Maendeleo ya Waislamu, n.k.

85. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeshirikiana vizuri na Jumuiya za kiislam kama vile Uamsho na pamekuwa na maendeleo mazuri baada ya pande hizi mbili kukutana. Hivi sasa Wizara inaendelea na taratibu za mazungumzo na Jumuiya ili kufikia muafaka mzuri kwa misingi ya utawala bora. Aidha Afisi ya Mufti imechukua hatua ya kutoa elimu kwa njia ya radio na televisheni kuhimiza viongozi wa dini kulinda amani na utulivu uliopo nchini.

86. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2003/2004, Afisi ya Mufti ilipata nafasi za Hijja kumi na sita (16), kulinganisha na nafasi kumi na tano (15) za mwaka 2002/2003. Kutokana na muda uliopewa Afisi ya Mufti kuwa mfupi, ilishindikana kuzigawa nafasi hizo kiwilaya kama ilivyokusudiwa na kulazimika kuchukua orodha iliyokuwepo na kuzigawa kufuatana na orodha hiyo. Pamoja

na hayo, Afisi ya Mufti inaendelea kutafuta tiketi za Hijja kutoka kwa wafadhili mbalimbali wa ndani na nje ya nchi.

87. Mheshimiwa Spika, Katika juhudi za kukuza elimu ya dini kwa usawa, Afisi ya Mufti imepiga hatua kwa kuanzisha na kuviendeleza vipindi vya akinamama katika televisheni ya Zanzibar. Nia ni kuvitangaza vipindi kama hivyo katika Sauti ya Tanzania Zanzibar kwa kuzingatia kuwa watu wengi hawana televisheni.

88. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha hadi kufikia mwezi wa Machi 2004 Idara imepokea wageni mbalimbali akiwemo Rais wa "World Muslim Congress", Mufti wa Oman, Mjumbe wa Vatican, Ujumbe wa Libya, n.k. Aidha ziara nne(4) zimefanyika nje ya nchi. Miongoni mwa ziara hizo ni zile zilizomshirikisha Mheshimiwa Mufti katika nchi ya Ufaransa. Hii ni katika kudumisha mashirikiano na taasisi mbalimbali.

89. Mheshimiwa Spika, juhudi za kuipatia Afisi ya Mufti jengo la kudumu zinaendelea. Kuna matumaini kwa Serikali ya Oman kusaidia ujenzi huo, kwa maelekezo ya kutumia mchoro wa ramani ya Afisi yao na pia kubadilisha kiwanja kutoka kile cha nyuma ya soko la Mwanakwerekwe hadi maeneo ya Mazizini.

90. Mheshimiwa Spika, ninayo furaha kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi imeshatoa kiwanja hapo Mazizini baina ya majengo ya Wizara ya Elimu. Kiwanja hicho kina ukubwa wa mita za mraba elfu tatu 3000 (3000sqm) na kinatosha kujenga ofisi hiyo kwa mujibu wa ramani iliyoletwa. Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi inatayarisha hati rasmi ya kiwanja hicho.

91. Mheshimiwa Spika, kazi za utafiti hasa zinazofanywa na wageni mbalimbali zimeendelea. katika kipindi cha mwaka 2003/2004 jumla ya tafiti 3 zilifanyika. Miongoni mwao ni utafiti wa ndoa za Kiislamu, jinsi Uislamu ulivyoingia Zanzibar na mtazamo wa Uislamu katika mapambano dhidi ya UKIMWI.

92. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004 Idara imewaendeleza wafanyakazi wake wane (4), kati ya hao mwanamme moja anaendelea na mafunzo Nchini Sudan kwa kiwango cha PhD na wanawake watatu (3) wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi hapahapa nchini. Aidha Idara imepata mashine moja ya Fax kwa kuongeza ufanisi wa kazi.

93. Mheshimiwa Spika, Shirika la Mpango wa Misaada la Umoja wa Mataifa UNDP limeisaidia Afisi ya Mufti kwa kuwaendeleza wafanyakazi kupitia kozi za muda mfupi. Vile vile inatarajia kupata vifaa vya afisi toka kwa wafadhili hao. Tunachukua nafasi hii kuwashukuru kwa misaada yao ambayo itasaidia kuongeza ufanisi.

94. Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yote yaliyopatikana, bado Idara ya Mufti wa Zanzibar inaendelea kukabiliana na matatizo yafuatayo:-

(i) uhaba wa vitendea kazi;

(ii) uhaba wa wafanyakazi wenye taaluma ya kutosha; na

(iii) uhaba wa vifaa vya mawasiliano.

95. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2004/2005 Idara ya Mufti wa Zanzibar imejiwekea malengo yafuatayo:-

(i) kuendeleza juhudi za kupata jengo jipya la Afisi ya Mufti ;

(ii) kuendeleza juhudi za kutoa taaluma kwa Masheikh, Maimamu, Wanazuoni na wananchi kwa jumla juu ya umuhimu wa Amani na Utulivu Nchini ;

(iii) kuendelea na kazi ya utoaji wa Fatwa na utatuzi wa migogoro inayowahusu Waislamu; na

(iv) Kuendelea na juhudi za kuwapatia wafanyakazi wake taaluma mwafaka.

96. Mheshimiwa Spika, ili Idara hii iweze kutekeleza kazi zake kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2004/2005, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi milioni tisini na mbili ,laki nne na tisini na mbili elfu (92,492,000) kwa ajili ya kazi za kawaida.

IDARA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

97. Mheshimiwa Spika, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni taasisi muhimu katika kuimarisha misingi ya Utawala Bora kama

ilivyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020 pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2000. Katika kipindi cha 2003/2004 Idara imeendelea kufanya kazi zake kwa mujibu wa kifungu No. 112 (3) cha Katiba ya Zanzibar na kwa mujibu wa sheria ya kuanzishwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, sheria namba 11 ya mwaka 2003. Jukumu kubwa la Afisi hii ni kuzifanyia ukaguzi fedha zote zinazotolewa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali na baadae kutoa taarifa zake za ukaguzi katika Baraza la Wawakilishi.

98. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Afisi imefanikiwa kukamilisha na hatimae kupitishwa kwa Sheria namba 13 ya mwaka 2003 ya uanzishwaji wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kupitishwa kwa Sheria hii kunaipa uwezo zaidi Afisi kutekeleza vyema malengo yake.

Ripoti za Ukaguzi

99. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004 Afisi imewasilisha Ripoti ya Ukaguzi wa mahesabu ya mwaka 2000/2001 na tayari ripoti hiyo imewasilishwa katika Baraza lako tukufu na imeshafanyiwa kazi na Kamati ya Kuchunguza Mahesabu ya Serikali (PAC). Kamati iliwasilisha ripoti katika kikao kilichopita cha mwezi wa Machi hadi April, 2004. Aidha matayarisho ya kitabu cha ripoti ya mahesabu kwa kipindi cha mwaka 2001/2002 yako katika hatua za mwisho kukamilika na itawasilishwa Serikalini na katika Baraza lako tukufu wakati wowote kuanzia sasa.

100. Mheshimiwa Spika, Afisi imekamilisha kazi za ukaguzi wa mahesabu ya mwaka 2002/2003 na ripoti za ukaguzi huo zimewasilishwa katika taasisi mbalimbali kwa kujibiwa. Mara tu majibu hayo yatakapokamilika kazi za utayarishaji wa kitabu cha ripoti zitaanza. Vile vile kazi ya ukaguzi wa mahesabu kwa kipindi cha mwaka 2003/2004 zimeshaanza kwa baadhi ya taasisi za Serikali na inatarajiwa kazi hiyo itamalizika na hatimae ripoti kuwasilishwa kwa wakati.

Mafunzo na Maendeleo ya Wafanyakazi

101. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004 malengo mengi ya Idara yametekelezwa kwa ufanisi mkubwa na kuleta matumaini ya kuongezeka kwa kiwango cha utekelezaji wa Afisi kwa ujumla. Afisi imewapatia wafanyakazi wake wanne (4) mafunzo huko Tanzania Bara. Mafunzo hayo yalipatikana kwa mashirikiano yaliyopo baina yetu na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Tanzania Bara. Vile vile jumla ya

wafanyakazi thalathini (30) wa ngazi ya uongozi na wakaguzi ishirini na tatu (23) wa kawaida wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ya ukaguzi yakinifu kwa nyakati tafauti.

Ukaguzi katika Halmashauri za Wilaya

102. Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2003/2004 nilieleza juu ya kuanzisha ukaguzi katika Halmashauri za Wilaya. Ukaguzi huo unaendelea na taarifa zake zitawasilishwa katika Baraza lako tukufu mara tu baada ya kukamilika kwake. Hatua hii ni changamoto katika harakati za kuondoa umaskini. Sambamba na hilo, Afisi imeweza kuongeza idadi ya wafanyakazi kwa Afisi ya Pemba na Mikoani. Hivi sasa tayari jumla ya wafanyakazi kumi na nne (14) wakiwemo wanawake kumi (10) na wanaume wanne (4) wameshaajiriwa kwa ajili ya Mikoani na wafanyakazi (30) kwa Afisi ya Pemba. Hali hii inaimarisha utendaji kazi wa Afisi.

Maazimio kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005

103. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2004/2005 Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inakusudia kuimarisha mahusiano yaliyopo kati yake na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Tanzania Bara. Mahusiano hayo yanahusu maeneo mbalimbali yakiwemo ya mafunzo ya kazi kwa vitendo, mafunzo kwa njia ya semina na kadhalika.

104. Mheshimiwa Spika, Afisi hii pia itaanzisha rasmi utekelezaji wa ukaguzi yakinifu (Performance Auditing or Value for Money Audit). Ukaguzi yakinifu unakusudia kufanyika kwa taasisi zote za Serikali kwa upande wa mapato na matumizi. Mkazo zaidi utatiwa katika upande wa ukusanyaji mapato na kuchunguza kwa kina sababu zinazopelekea taasisi nyingi za Serikali kushindwa kufikia lengo la ukusanyaji wa mapato. Hii ni kwa vile tatizo hili linaongezeka siku hadi siku.

105. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pia inakusudia kuongeza nguvu zaidi kufanya ukaguzi katika sehemu za mapato. Hili litatekelezwa kwa kuangalia vianzio mbalimbali vya mapato. Aidha Afisi hii inatarajia kuanzisha kitengo maalum cha kushughulikia ukaguzi wa mapato, ambacho kitahusika pia na kufanya tathmini ya ukusanyaji kwa kulinganisha makadirio ya mapato kwa mwaka na makusanyo halisi. Hoja za ukaguzi zitatolewa pale panapobainika tofauti. Kuwepo kwa kitengo hiki kutasaidia kubaini pia mianya ya uvujaji wa mapato na hivyo kuweka mikakati ya kuiziba.

106. Mheshimiwa Spika, kwa vile Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inapania kuanzisha kitengo hiki cha ukaguzi yakinifu hatua mbalimbali zimeshaanza kuchukuliwa kuhakikisha kwamba kazi hiyo itafanyika ipasavyo. Baadhi ya hatua hizo ni kuwapatia mafunzo wakaguzi kuhusu dhana nzima ya ukaguzi yakinifu.

107. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005 Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

(i) kuendeleza mashirikiano yaliyopo baina ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Muungano ya Tanzania na Afisi yetu ya Zanzibar katika nyanja za masomo ya ndani ya vitendo na kushirikiana katika ukaguzi kwa Taasisi za Serikali ya Muungano zilizopo Zanzibar;

(ii) kuendelea kutekeleza mradi wa Uimarishaji wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

(iii) kuendelea kuweka mazingira mazuri ya wafanyakazi;

(iv) kuwaendeleza kitaaluma wafanyakazi wa Afisi ndani na nje ya nchi; na

(v) kutayarisha kanuni mbalimbali za utekelezaji na kuipa nguvu Sheria Namba 11 ya mwaka 2003 ya kuanzishwa kwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

108. Mheshimiwa Spika, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hadi kufikia mwezi wa Machi 2004 imeweza kukusanya jumla ya Shilingi milioni moja(1,000,000). Katika kipindi cha mwaka 2004/2005 Afisi imekusudia kukusanya na kuchangia katika mfuko Mkuu wa Serikali jumla ya Shilingi milioni moja na laki tano (1,500,000)

109. Mheshimiwa Spika, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili iweze kutekeleza malengo ya kazi zake kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2004/2005 naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi milioni mia nne na sitini na nne (464,000,000) kwa kazi za kawaida na Shilingi milioni ishirini na moja (21,000,000) kwa kazi za maendeleo.

MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA KUSIMAMIA MAADILI YA VIONGOZI

110. Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2003/2004 wakati nikiizungumzia Taasisi ya Kupambana na Rushwa kwamba, muelekeo wa Taasisi hiyo kikazi na kimajukumu ulilenga zaidi matokeo ya uchambuzi wa kitaalamu uliotokana na Mpango wa miaka mitano wa Utawala Bora wa Zanzibar na uchambuzi wa kina wa kazi za Wizara uliofanywa na washauri chini ya utekelezaji wa mpango huo. Kufuatia uchambuzi huo imeonekana ipo haja ya Taasisi ya Kupambana na Rushwa na ile ya Kusimamia Maadili ya Viongozi kuunganishwa na kuwa Mamlaka moja yenye jina la *"MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA KUSIMAMIA MAADILI YA VIONGOZI".*

111. Mheshimiwa Spika, kuna sababu nyingi za kukubaliana na shauri hilo lakini kuu ni mbili. Kwanza kazi za Taasisi hizo zote zinaoana, zinafanana na zenye mwelekeo mmoja. Pili itasaidia kupunguza gharama zisizo za lazima za uendeshaji.

112. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Wizara imeshaandaa rasimu ya sheria ya kuipa nguvu kiutendaji Mamlaka hiyo na hivi sasa rasimu hiyo inajadiliwa na wadau mbalimbali kabla ya kuletwa katika Baraza lako tukufu. Ili kuwa na wataalamu wenye kukubalika katika mamlaka hiyo Wizara imeshawapeleka wafanyakazi wane(4) Chuo Kikuu cha Zanzibar kusomea fani ya Uchumi na Sheria.

113. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005 Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Kusimamia Maadili ya Viongozi imelenga kutekeleza malengo yafuatayo:-

(i) kuendelea na kazi ya ukamilishaji wa Sheria ya Mamlaka;
(ii) kuchambua muundo wa Mamlaka;

(iii) kuwaendeleza wafanyakazi kitaaluma; na

(iv) kujenga miundo-mbinu ya kiutendaji.

114. Mheshimiwa Spika, ili Mamlaka hii iweze kutekeleza vyema majukumu yake katika kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005 naliomba

Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi milioni mia moja ishirini na sita, laki mbili na arubaini na nne elfu(126,244,000) kwa kazi za kawaida.

IDARA YA KURATIBU SHUGHULI ZA UTAWALA BORA

115. Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwamba Wizara yetu ililazimika kufanya tathmini na utafiti kuhusu kazi na majukumu ya taasisi zake hasa zile zilizo chini ya utendaji wa Katibu Mkuu. Katika tathmini hiyo ilionekana ipo haja ya kuwa na Idara hii muhimu na pia kuiondoa Taasisi ya Kusimamia Haki za Binaadamu hasa kwa vile sehemu kubwa ya kazi zake zitafanywa na Tume ya Haki za Binaadamu ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. Baadhi ya kazi ambazo zingefanywa na Taasisi ya Haki za Binaadamu hapa Zanzibar zitafanywa na Idara hii.

116. Mheshimiwa Spika, majukumu makuu ya Idara hii ni pamoja na:-

(i) kuratibu kazi na shughuli zote za Utawala Bora katika taasisi zote;

(ii) kuchambua na kutoa tathmini juu ya Kiwango cha Utawala Bora;

(iii) kuanzisha na kurekebisha viashiria (indicators) vya utawala bora na kuvipima;

(iv) kuendeleza kazi ya uimarishaji utawala bora;

(v) kuratibu shughuli za NGOs; na

(vi) kuratibu shughuli za haki za binaadam.

117. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005 Idara imejiwekea malengo yafuatayo:-

(i) Kuendelea na kazi ya uundwaji wake.

(ii) Kuendelea na juhudi za kuipatia vifaa vya kiutendaji;

(iii) Kuimarisha nguvukazi yenye taaluma; na

(iv) Kusimamia utekelezaji wa majukumu yake makuu.

118. Mheshimiwa Spika, ili Idara hii iweze kutekeleza vyema majukumu yake katika kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005 naliomba Baraza lako

tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi milioni hamsini na mbili laki sita na hasini elfu (52,650,000) kwa kazi za kawaida.

AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

119. Mheshimiwa Spika, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka bado ni afisi mpya iliyoanzishwa miaka miwili iliyopita na kupewa majukumu yake chini ya Katiba na Sheria mbalimbali. Majukumu hayo ni pamoja na kushughulikia uendeshaji wa kesi za jinai, kutoa ushauri wa kisheria na maelekezo kwa Jeshi la Polisi kuhusiana na upelelezi wa jinai na kuidhinisha kufanyika kwa uchunguzi wa tuhuma za jinai kwa baadhi ya makosa pamoja na kusimamia maslahi ya Taifa katika kuona haki inatendeka na kuhakikisha matumizi bora ya vyombo vya Dola.

120. Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha Afisi hii iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kila siku, mkazo ukiwa ni kuimarisha Afisi, kujenga misingi ya ufanisi wa kazi na kutekeleza malengo ambayo ilijipangia. Kati ya mwezi wa Julai 2003 na April 2004, Afisi hii imepokea jumla ya majalada mia mbili na thamanini na tano (285) ya kesi kutoka Polisi na kuyatolea maelekezo na uamuzi ikilinganishwa na majalada mia moja na sabiini na tatu (173) ya liyopokelewa katika kipindi kama hicho katika mwaka uliopita. Katika kipindi hicho hicho Afisi imesimamia jumla ya kesi hamsin (50) za rufaa. Aidha jumla ya kesi arubaini na tatu (43) za mauaji zimefunguliwa. Kati ya hizo kesi nane (8) ni za kuua kwa kukusudia,thalathini na nne (34)ni za kuua bila ya kukusudia na kesi moja ya kujaribu kuua. Kati ya kesi hizo arubaini na tatu (43) za mauaji, kesi kumi na saba (17) ni za ajali barabarani. Afisi pia imepokea malalamiko mia moja na hamsini na moja (151) yaliyohusu ama tuhuma za kuonewa au kutumika vibaya kwa madaraka ya Polisi, ucheleweshwaji wa kesi na kutoshughulikiwa kesi ipasavyo. Kwa mashirikiano na Jeshi la Polisi na Mahkama, Afisi imeweza kuyatatua baadhi ya malalamiko hayo kwa kiwango cha kuridhisha.

121. Mheshimiwa Spika, katika kuiimarisha Taasisi hii, Afisi ilitafuta na kupata msaada wa vitabu mbalimbali vya Sheria, kuweka mtandao wa ndani wa kompyuta *'Local Area Network'* ambapo kompyuta sita zimeunganishwa katika mtandao huo. Aidha Afisi imeweza kupata mashine moja ya fotokopi, mashine mbili za kunakili picha na nyaraka *'scanners'*, vipando viwili aina ya vespa na gari moja jipya. Pia Afisi iliweza kuwapatia mafunzo wafanyakazi wake wanne ndani ya nchi na mmoja nje ya nchi.

122. Mheshimiwa Spika, mbali na kutekeleza kazi za kawaida kama nilivyozieleza, Afisi pia ilitekeleza malengo iliyojiwekea kwa mwaka wa fedha unaomalizika wa 2003/2004 kama ifuatavyo:

Kuajiri wanasheria na watendaji wengine

123. Mheshimiwa Spika, Wanasheria ndio nguzo muhimu ya Afisi katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku. Afisi ilijiwekea lengo la kuajiri wanasheria kumi (10) ambapo kati ya hao wanasheria saba (7) wameshaajiriwa na wanaendelea na kazi. Wanasheria watatu (3) waliobaki pamoja na watendaji wengine wanatarajiwa kuajiriwa katika mwaka ujao wa fedha baada ya kukamilika matengenezo ya sehemu za jengo zilizobaki ili kutoa nafasi kwa wafanyakazi hao wapya.

Mafunzo ya vitendo kwa wanasheria

124. Mheshimiwa Spika, kutokana na upya wa wanasheria wetu katika kazi za uendeshaji wa mashtaka, suala la mafunzo ya vitendo limekua na umuhimu wa pekee ili kujijengea uwezo na hatimae kuweza kumudu kazi zao kwa ufanisi na kujiamini zaidi. Wanasheria wanne (4) wamepatiwa mafunzo hayo kwa awamu ya kwanza ambapo wawili wamepelekwa katika Mahakama Kuu Dodoma na wawili Mahakama Kuu Dar es Salaam. Katika awamu ya pili wanasheria wengine watatu (3) walipelekwa katika mafunzo kama haya ambapo wawili wamepelekwa katika mahakama ya Morogoro na mmoja katika mahakama iliyoko Biharamulo.

Upatikanaji wa Majengo ya Afisi

125. Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika hotuba yangu ya mwaka jana kuwa jengo la ghorofa moja kwa ajili ya Afisi hapa Unguja limeshapatikana na kwa kuanzia ghorofa ya chini inatumika na vifaa muhimu vya kutendea kazi vimewekwa. Sehemu ya juu ya jengo inatarajiwa kufanyiwa marekebisho hivi karibuni baada ya afisi iliyokuwa ikitumia sehemu hiyo kuhama. Kutokana na uhaba wa fedha, hatua za kupata jengo kwa ajili ya afisi za Pemba zitaendelezwa katika mwaka ujao wa fedha.

Utunzaji wa kumbukumbu za kimahkama

126. Mheshimiwa Spika, ukusanyaji na uwekaji wa taarifa za uendeshaji mashtaka pamoja na taarifa nyengine zinazohusiana na hili ni eneo muhimu katika utekelezaji wa kazi za kila siku za Afisi hii. Kazi hii imeanza rasmi mwezi Januari 2003, na kwa kushirikiana na UNDP, Afisi katika mwaka ujao

wa fedha imeandaa mpango maalumu ikiwemo upatikanaji wa nyenzo za kufanyia kazi zitakazowezesha kazi hii kufanywa kwa ufanisi zaidi.

Tathmini ya taratibu za uendeshaji mashtaka

127. Mheshimiwa Spika, usimamizi na uendeshaji wa masuala ya jinai ni moja kati ya majukumu ya Kikatiba ya Afisi hii. Ili kulitekeleza hilo, Afisi imefanya mikutano na wadau mbalimbali wa Sheria kama Mahakama, Jeshi la Polisi na Wanasheria wa kujitegemea kupitia na kutathmini taratibu zilizopo za uendeshaji mashtaka na kutoa mapendekezo ya kurekebisha kasoro zilizopo. Mkutano mwingine utafanyika mwezi wa Disemba mwaka huu ili kutathmini utekelezaji wa mapendekezo ya mkutano wa awali.

Mapitio ya Sheria ya Jinai Sura ya 13 na Sheria ya Nyendo za Jinai Sura ya 14

128. Mheshimiwa Spika, suala la kuzifanyia mapitio sheria hizi mbili lilionekana kuwa ni jambo la lazima ili matumizi yake yaweze kuendana na wakati huu tulionao, hatua mbalimbali zilichukuliwa kufanikisha azma hii. Wadau wa sheria walishiriki kikamilifu mikutano ya kupitia na kujadili ripoti na mapendekezo yaliyotolewa na wataalam. Nina furaha kulieleza Baraza lako tukufu kuwa matunda ya utekelezaji wa lengo hili ni mswaada wa marekebisho ya sheria hizo uliowasilishwa Barazani kwa kujadiliwa na hatimae kupitishwa katika kikao kilichofanyika mwezi wa Machi 2004.

129. Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya mwaka jana vile vile nilieleza kuwa muelekeo wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ni kuleta ufanisi katika uendeshaji mashtaka ili wananchi waweze kutoa ushirikiano kwa vyombo vinavyohusika na usimamizi wa sheria. Katika kutekeleza hili Wanasheria wa Afisi hii wameshaanza kazi za uendeshaji mashtaka katika Mahakama za Mkoa Vuga na baadae utaratibu huo utaendelea katika Mahkama za Mikoa mengine. Lengo ni kuhakikisha kuwa uendeshaji wa kesi za jinai katika Mahkama zote za Mkoa unafanywa na wanasheria wa Afisi hii.

130. Mheshimiwa Spika, katika kufanikisha kazi zake, Afisi imekuwa ikipata mashirikiano makubwa kutoka taasisi na vyombo mbalimbali vya ndani na nje ya nchi. Afisi imekuwa ikifanya kazi zake kwa mashirikiano ya karibu na UNDP, Sekreterieti ya Jumuiya ya Madola na Shirika la Umoja wa Mataifa la kuzuia Uhalifu na Madawa ya Kulevya. Aidha Afisi imeanzisha Mawasiliano na Umoja wa Kimataifa wa Waendesha Mashtaka.

131. Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana lakini bado Afisi hii ni mpya na hivyo inahitaji kuendelezwa kwa kupatiwa nyenzo na fedha za kufanyia kazi ili kuleta ufanisi uliokusudiwa. Hata hivyo hali imekuwa ni tofauti kwani upatikanaji wa fedha umekuwa hauridhishi na kukwamisha utekelezaji wa kazi. Kati ya Shilingi milioni mia moja na hamsini na mbili (152,000,000) zilizotengwa kwa kuendeshea kazi kwa kipindi cha mwaka 2003/2004 ni Silingi milioni sabiini,laki tano na tisini na mbili elfu. (70,592,000) sawa na asilimia arobaini na sita (46%) tu ndizo zilizopatikana hadi kufikia mwezi April 2004. Kati ya fedha hizo shilingi milioni arubaini na saba,laki moja natisini na mbili elfu (47,192,000) sawa na asilimia sitini na saba (67%) zimelipwa mishahara na maposho na shilingi milioni kumi na tisa,laki nne na kumi na tisa elfu (19,419,000) zilitumika kwa matengenezo ya Afisi na ununuzi wa samani na vifaa vyengine vya Afisi kabla ya kuhamia na shilingi milioni tatu,laki tisa na thamanini na moja elfu (3,981,000) tu ndizo zilizopatikana kwa kuendeshea Afisi.

132. Mheshimiwa Spika, Afisi hii inakabiliwa na matatizo yafuatayo :-

(i) uhaba wa vifaa vya kazi;

(ii) uhaba wa nyenzo; na

(iv) mazingira yasiyoridhisha ya jengo.

133. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, Afisi imejiwekea malengo yafuatayo:

(i) utekelezaji wa mpango wa uimarishaji wa huduma za maktaba kwa kuajiri mkutubi, kutafuta vitabu na majarida na kuweka mtandao wa mawasiliano ili huduma hizo pia zipatikane kwa njia ya kisasa ya elektroniki (electronic library) ;

(ii) utayarishaji muongozo wa uendeshaji wa kesi (prosecution manual);

(iii) kutafuta jengo kwa ajili ya Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka huko kisiwani Pemba;

(iv) kuchapisha na kusambaza kwa wahusika Sheria mpya za Jinai na nyendo za Jinai ambazo zimepitishwa na Baraza lako hili tukufu katika kikao kichofanyika mwezi Machi, 2004;

(v) kuimarisha Afisi ya Uendeshaji Mashtaka Vuga kwa kuipatia vitendea kazi;

(vi) kukamilisha utaratibu wa mashtaka kuendeshwa na Wanasheria wa Afisi hii kwa Mahkama zote za Mikoa, Unguja; na

(vii) Kuwapatia mafunzo wafanyakazi wa Afisi hii.

134. Mheshimiwa Spika, ili Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka iweze kutekeleza vyema malengo iliyojiwekea katika kipindi cha 2004/2005, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi milioni mia moja na sabiini na saba (177,000,000) kwa kazi za kawaida.

IDARA YA MWANASHERIA MKUU

135. Mheshimiwa Spika, Idara ya Mwanasheria Mkuu katika mwaka wa fedha wa 2003/2004 iliendelea na utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba ya Zanzibar na malengo iliyojiwekea. Idara ya Mwanasheria Mkuu imegawika katika sehemu kuu mbili zifuatazo:-

(A) AFISI YA MWANASHERIA MKUU; na

(B) TUME YA KUCHUNGUZA SHERIA.

136. Mheshimiwa Spika, majukumu ya msingi ya kazi za Afisi ya Mwanasheria Mkuu ni:-

(i) kuwa mshauri mkuu wa kisheria kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

(ii) kutekeleza shughuli nyengine zozote za kisheria zitazopelekwa kwake au zitakazoagizwa na Rais wa Zanzibar; na

(iii) kutekeleza shughuli zozote za kisheria kwa mujibu wa masharti ya Katiba au sheria nyenginezo zozote.

137. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2003/2004, Afisi ya Mwanasheria Mkuu iliweza kutekeleza majukumu yake kwa kiwango cha kuridhisha. Katiba na sheria nyingine mbalimbali

zimeimarishwa kwa ajili ya kukuza Demokrasia na Utawala Bora katika nchi yetu.

138. Mheshimiwa Spika, kazi za uandishi wa Sheria za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mwaka wa fedha wa 2003/2004 ilifanywa kwa ufanisi mkubwa. Jumla ya Miswada ya Sheria 14 imetayarishwa na kuwasilishwa katika Baraza lako tukufu kulinganisha na Miswada ya Sheria 12 katika mwaka wa fedha wa 2002/2003; hili ni sawa na ongezeko la asilimia 15%. Miswada ya Sheria hizo husika ni:-

(i) Mswada wa Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali kwa mwaka wa 2003/2004;

(ii) Mswada wa Sheria ya Fedha;

(iii) Mswada wa Sheria ya Kuanzishwa Tume ya Utumishi ya Mahkama;

(iv) Mswada wa Sheria ya Kulinda Hati Miliki na Haki Shiriki;

(v) Mswada wa Sheria ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya;

(vi) Mswada wa Sheria ya Uanzishwaji wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

(vii) Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Uchaguzi;

(viii) Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Tume ya Utumishi wa Baraza la Wawakilishi;

(ix) Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Matumizi ya Ardhi;

(x) Mswada wa Sheria ya Kufuta na Kuanzisha Upya Sheria ya Baraza la Taifa la Kiswahili;

(xi) Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kikosi Maalum cha Kujitolea na Kuanzisha Kikosi cha Volantia;

(xii) Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Utaratibu wa Kuendesha Kesi za Jinai;

(xiii) Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Jinai. na

(xiv) Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Vipimo na Mizani

139. Mheshimiwa Spika, aidha Afisi ya Mwanasheria Mkuu imeandika matangazo mengine mbalimbali ya kisheria (Legal Notices) hamsini na nne (54), na kusimamia (kwa niaba ya Serikali) kesi ishirini na mbili (22) za Madai. Vile vile, Afisi ilipokea malalamiko arubaini na tano (45) ya wananchi ambayo yalipatiwa ushauri na maelekezo ya kisheria.

140. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004 juhudi ya kuwapatia elimu na ujuzi wa ziada wafanyakazi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu zimefanikiwa vizuri. Wanasheria wawili (2)wamepatiwa nafasi ya masomo ya juu (Shahada ya Pili) LL.M nchini Uingereza na Afrika ya Kusini. Aidha wafanyakazi ishirini na saba (27) wamepatiwa mafunzo ya kompyuta hapa Zanzibar. Katika mwaka wa fedha wa 2004/2005 Afisi inakusudia kuwapatia elimu ya ziada wafanyakazi wanne(4); mmoja atapatiwa nafasi ya masomo ya Shahada ya Pili ya Sheria (LL.M) na watatu (3) mafunzo ya muda mfupi ya Uandishi wa Sheria (Legislative Drafting) na Usuluhishi wa Migogoro (Arbitration).

141. Mheshimiwa Spika, vile vile katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2003/2004, Afisi ya Mwanasheria Mkuu imeweza kuajiri wanasheria wawili (2)waliomaliza mafunzo yao katika Chuo Kikuu cha Zanzibar. Aidha Afisi inategemea kuwapokea wafanyakazi wengine wawili baada ya kumaliza masomo yao mwishoni mwa mwaka wa 2004.

142. Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo mazuri ya kiutendaji katika kipindi hicho, Afisi ya Mwanasheria Mkuu inaendelea kukabiliwa na matatizo mengi ikiwa ni pamoja na:-

(i) uhaba wa Wanasheria wenye uzoefu wa kazi;

(ii) uchache wa vifaa vya kufanyia kazi, mfano vitabu vya Rejea vya Sheria;

(iii) ukosefu na uhaba wa huduma muhimu za usafiri na mawasiliano ya kisasa ya “internet”; na

(iv) uhaba wa nafasi za Afisi kwa ajili ya wafanyakazi kutokana na udogo wa jengo.

143. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2004/2005, Afisi ya Mwanasheria Mkuu inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

(i) kuendelea kuishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa misingi ya Katiba, kwa hekima na busara;

(ii) kuendelea na utayarishaji wa Miswada ya Sheria pamoja na matangazo mbalimbali ya kisheria;

(iii) kusimamia shughuli za uchapishaji wa Sheria pamoja na matangazo mbalimbali;

(iv) kuwapatia elimu ya ziada wafanyakazi wa kada mbalimbali;

(v) kuzidisha juhudi ya kupata vifaa vya kufanyia kazi, ikiwa ni pamoja na njia za mawasiliano ya kisasa; na

(vi) kuendelea na usimamizi (kwa niaba ya Serikali) wa Kesi za Madai Mahkamani.

(B) TUME YA KUCHUNGUZA SHERIA

144. Mheshimiwa Spika, Tume ya Kuchunguza sheria ni sehemu ya pili muhimu ya Idara ya Mwanasheria Mkuu. Tume hiyo imeanzishwa kwa Sheria Namba 16 ya 1986 na imepewa majukumu ya kuchunguza sheria mbalimbali na kupendekeza marekebisho ambayo yanaendana na mabadiliko ya kukua kwa Demokrasia na Utawala Bora katika nyanja za siasa, uchumi na ustawi wa jamii katika nchi yetu.

145. Mheshimiwa Spika, majukumu hayo ya Tume yanaweza tu kutekelezwa kwa ufanisi na jopo la Wanasheria waliokomaa (wazoefu) katika kazi za uanasheria. Kama nilivyoeleza katika Hotuba yangu ya mwaka jana 2003/2004, Tume haikuweza kufanyakazi zake kwa ufanisi kutokana na upungufu mkubwa wa wataalamu hao.

146. Mheshimiwa Spika, baada ya kufanywa juhudi kubwa, Tume imekwishapatiwa Mwenyekiti mpya mzalendo tokea tarehe 10 Septemba, 2003 ili kuziba pengo lililoachwa wazi na raia wa Nigeria aliyoamua ghafla

kurudi kwao. Wizara yangu kwa mashirikiano na Mwenyekiti wa Tume hiyo na kwa msaada wa UNDP chini ya Mradi wa Uimarishaji wa Utawala Bora inaandaa mikakati ya kuihuisha Tume ili iweze kufanya kazi zake ipasavyo katika mwaka wa fedha 2004/2005 kwa:-

(i) kuipatia tume Afisi rasmi badala ya kuwa na Afisi za mshikizo;

(ii) kupata wataalamu (Makamishna) na wafanyakazi wengine; na

(iii) kuipatia Tume nyenzo za kufanyia kazi.

147. Mheshimiwa Spika, ili Idara ya Mwanasheria Mkuu iweze kutekeleza malengo iliyojipangia kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005 naliomba Baraza lako tukufu, liidhinishe Shilingi milioni mia tatu na mbili (302,000,000) kwa matumizi ya kazi za kawaida.

AFISI KUU PEMBA

148. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Afisi Kuu Pemba imeendelea na shughuli zake kama ilivyojipangia. Aidha imeweza kwa kiasi kikubwa kuunganisha kazi, maelekezo na shughuli mbalimbali ambazo ama zilitakiwa zifanywe kwa pamoja au zitekelezwe na Afisi Kuu. Pamoja na hayo imesaidiana na Makao Makuu ya Wizara katika kuratibu mafunzo na Semina zinazohusu Utawala Bora kwa wajumbe kutoka Pemba.

149. Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kuwaendeleza wafanyakazi kitaaluma, Afisi Kuu kwa mwaka 2003/2004 imempeleka mafunzoni mfanyakazi mmoja na kuajiri mfanyakazi mmoja. Aidha kazi za matengenezo ya jengo la afisi nayo imeendelea kwa kiwango cha kuridhisha. Shughuli za uratibu wa NGO's zimeendelea vizuri ambapo kitengo kimetoa elimu kwa Jumuiya zisizo za kiserikali kuelewa umuhimu wa kuwa na katiba zao na kuziheshimu. Aidha wafadhili mbalimbali wamejitokeza kuzisaidia Jumuiya hizo.

150. Mheshimiwa Spika, ijapokuwa Afisi Kuu – Pemba imefanikiwa katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali, pia yapo matatizo yanayorejesha nyuma ufanisi bora wa kazi zake, kama vile:

(i) uhaba na ubovu wa vyombo vya usafiri;

(ii) uhaba wa wafanyakazi wenye taaluma; na

(iii) uhaba wa vitendea kazi.

151. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha fedha 2004/2005 Afisi Kuu Pemba inatarajia kutekeleza malengo yafuatayo:-

(i) kumaliza utengenezaji wa jengo katika hatua iliyobakia;

(ii) kununua vifaa vya afisini pamoja na vyombo vya usafiri kwa ajili ya wafanyakazi;

(iii) Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi pamoja na Semina mbalimbali; na

(iv) kukipatia nyenzo Kitengo cha Elimu ya Uraia ili kiweze kutoa Elimu kwa wananchi kupitia Semina, Vyombo vya Habari na Mikutano.

152. Mheshimiwa Spika. ili Afisi Kuu Pemba iweze kutekeleza na kusimamia vyema malengo iliyojiwekea kwa mwaka 2004/2005. Naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi milioni mia nne na mbili,laki moja na thamanini na moja elfu (402,181,000) kwa matumizi ya kazi za kawaida.

MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA MWAKA 2004/2005

153. Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza kazi za kawaida na maendeleo Wizara yangu inaomba jumla ya Shilingi bilioni tatu,na mia tatu na kumi na saba milioni (3,317,000,000) kwa kazi za kawaida na Shilingi milioni arubaini na moja ,laki nane na arubaini elfu (41,840,000) kwa kazi za maendeleo. Aidha naliomba Baraza lako pia likubali mchango wa Shilingi milioni mia moja na arubaini na sita,laki tano na arubaini elfu(146,540,000) ikiwa ni mapato yatakayokusanywa na Wizara hii ambayo yataingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali ***(ufafanuzi zaidi kiambatanisho M6.(i),(ii)(iii))***

MWISHO

154. Mheshimiwa Spika, kabla sijamaliza kusoma hotuba yangu hii kwa niaba yangu na watendaji wote wa Wizara yangu nawashukuru wajumbe wa

Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala ya Baraza lako hili tukufu. Hakika busara zao na ushauri wao ni hazina kubwa katika ufanisi wa kazi za Wizara yangu na suala zima la utayarishaji wa Bajeti ya Wizara yangu.
Aidha nawapongeza watendaji wote wa Wizara yangu kutokana na kuchapa kazi kwao na nawatakia kheri na kazi njema kwa mwaka unaofuata.

155. Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwashukuru wahisani, wafadhili na wadau wanaoshirikiana bega kwa bega na shughuli za Wizara. Naanza kwa kulishukuru Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Umoja wa Mataifa la *"World Intellectual Property Organisation"*(WIPO), Shirika la Kibinafsi la *"West Europe Computer", "Africa Muslim Agency", "Ali Yussuf Charitable" "Anga Khan Foundation", Nchi ya Oman, Qatar na Saudi Arabia* kwa misaada yao katika taasisi za Wizara yangu.

Aidha nazishukuru taasisi mbalimbali za ndani ya Zanzibar na Tanzania Bara kwa ushirikiano wao wa kuona kwamba ule wajibu na jukumu la kuimarisha misingi ya Utawala Bora linasimama. Sambamba na hilo nawashukuru wananchi wote wa Zanzibar kwa mashirikiano yao wanayoyatoa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu.

156. Mheshimiwa Spika, mwisho kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja.

BRIG. GEN. (Mst.) ADAM C. MWAKANJUKI
WAZIRI WA NCHI (AR)
KATIBA NA UTAWALA BORA
ZANZIBAR.